Mimi mwenyewe ninavyozungumza hapa, mimi ni skwota pale Kwale na mimi ni kiongozi. Kwa hivyo, ni furaha kwamba tuko wengi; kwamba nchi nzima inalilia suala hili. Waswahili husema: “Kilio cha wengi huwa ni harusi.” Kwa hivyo, nina imani kupitia taarifa hii na ripoti hizi, hususan hii ya Mwenda pale Taita Taveta, kwa sababu ni mahali ambapo nimeenda. Pia kuna ndugu zetu kutoka Kwale wanaokaa pale Mwanda na wako katika hatari hii ya kufurushwa kwao kwa sababu ya swala hili la ardhi.

Vile, nikirudi nyumbani, niseme ya kwamba suala hili limekidhiri sana katika Kaunti yangu ya Kwale. Nimeuliza kupitia kauli, taarifa kuhusu mashamba mengi ndani ya Kaunti ya Kwale. Nikutaarifu kwamba kuna wakaazi wa Wasini walioishi hapo zaidi ya miaka hamsini wakijua hapo ni kwao. Lakini leo hii kuna watu au familia binafsi na kwa sababu niko Bungeni leo na ninatetewa kisheria nikitaja majina, familia ya Saggaf imepata cheti cha ardhi ya Wasini pasipo kuwahusisha wananchi, viongozi wa Kaunti ya Kwale au Serikali ya Kaunti. Leo wanasema wanamiliki ardhi ya Wasini.

Vile vile, kuna hatari kuu sana ya wananchi wanaoishi sehemu ya Kuranzi, eneo bunge la Kinango. Wenyeji wana wasiwasi kwamba wakati wowote watafurushwa kutoka eneo lile. Inasemekana yupo bwenyenye anayemiliki ardhi ile.

Naomba serikali zetu za kaunti, najua kuna ugatuzi na wamepatia kipao mbele masuala mengine. Lakini kulingana na ripoti hizi, hususan ripoti ya Taita Taveva, serikali zetu za kaunti lazima zifanye bidii kuhakikisha zinalivulia njuga suala hili na kupambana nalo ili mwananchi asiyejiweza apate haki yake ya ardhi.

Itakuwa ni makosa sana iwapo tutashindwa kutatua suala la ardhi kama viongozi tuliowekwa uongizini. Kila siku tunapata malalamishi kwamba watu wanafukuzwa au nyumba zinabomolewa au watu ni *squatters* sehemu fulani. Hadithi hii ya squatter inafaa kufika kikomo. Namshukuru sana Sen. Faki kwa kazi nzuri na kujitolea kusafiri kila kona ya nchi hii kumsikiliza mwananchi na kuhakikisha anapata haki yake kupitia Kamati yake.

Bw. Naibu Spika, pia nakukumbusha kwamba baada ya Kamati za Seneti kufanya kazi na kutoa mapendekezo mazuri kama haya ambayo ni ya kufurahisha, yanayomjali mwananchi na ya kikatiba na kisheria, lakini Serikali yetu na asasi zake zinazembea kutekeleza mapendekezo haya. Itakuwa tumepoteza fedha nyingi za Serikali na mda mwingi ambao Sen. Faki na wanakamati wake wangepanya mambo yao ya kibinasi. Pengine wangeshughulikia masuala yao ya kisiasa au kukaa na jamii na familia zao, lakini wamejinyima mda ule ili kutuletea ripoti kama hii. Halafu, waliopo na jukumu la kutekeleza wajibu huo, wanashindwa kutekeleza mapendekezo ya Kamati zetu za Seneti.

Bw. Naibu Spika, nitakupa mfano. Hivi majuzi kabla tuende kwa likizo fupi, tulileta ripoti Bungeni ya kufidia wananchi wa Ramisi, vijiji vya Nikavu, Mkono wa Ndugu na vinginevyo. Walifaa kupewa ardhi mbadala ili waendeleo na maisha yao. Ilikuwa amri, wala sio pendekezo, ya mahakama kwamba tume ya masuala ya Ardhi, the NLC, ihakikishe wananchi wa Ramisi wamefidiwa na kupewa ardhi mbadala ili shughuli zao za kawaida ziendeleo. Jambo la kusikitisha ni kwamba hadi sasa, hilo halijafanyika.

Tujiulize, je kuna haja gani Seneti kuwekeza pesa kusafiri sehemu nchini kama Kilifi na Malindi? Vilevile nafahamu pale Malindi uwanja wa ndege, kuna *squatter* zaidi ya 1,000 eneo la Ganda wanaoishi katika hali ya sinto fahamu kwa sababu hawajui kama ni sehemu yao, ilihali wamejenga na wanaishi hapo na hata wanazikana kwa ile ardhi. Sio

sawa ikiwa ndugu yangu, Sen. Madzayo, ataenda kuomba kura tena kwa wananchi na suala hili halijashughulikiwa.

Naiomba Serikali Kuu na serikali za kaunti zitenge pesa kuhakikisha mapendekezo ya kugawanya ardhi hii yafanyike. Tunaona kuna ubadhirifu mwingi wa pesa katika serikali za kaunti, lakini hawafahamu kuna haja ya kuwekeza kuhakikisha wananchi wao wamepata ardhi na wanaishi mahali ambapo hawatasumbuliwa na mtu yeyote na wapate cheti cha ardhi yao.

Nikimalizia, kwa sababu hali hii ni halisia nchini kote, napongeza serikali ya mseto katika jukumu lake na juhudi zake za kuhakikisha kwamba suala la mashamba limetatuliwa pale pwani.

Leo hii wenzangu waliopo hapa, namuona Seneta wa Kaunti ya Taita Taveta pamoja na Sen. Faki na Sen. Madzayo, watakubaliana nami asilimia mia kwamba tuko katika mikakati ya kuhakikisha mashamba yote yaliochukuliwa na mabwenyenye na hawapo, tupate orodha ya *squatters* na kuwasilisha orodha hiyo kwa ofisi husika. Serikali kuu inafaa kulipa fidia ili watu wetu wa Kaunti ya Kilifi, Kwale, Mombasa, Tana River, Lamu na Taita Taveta wapewe ardhi yao ili waishi vizuri. Wakifanya hivyo, wananchi watafahamu kuwa Serikali yao ipo pamoja nao.

Bw. Naibu Spika, kwa hayo mengi au machache, asante sana. Napongeza Kamati ya Sen. Faki. Naamini hivi karibuni, nitahakikisha kuwa Kamati hii imefika Wasini, Kaunti ya Kwale, kuchunguza hatari iliyopo kutokana na masuala ya ardhi.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Senate Minority Leader, Sen. Madzayo.

The Senate Minority Leader (Sen. Madzayo): Asante sana, Bw. Naibu Spika. Naungana na Maseneta wenzangu waliochangia Hoja hii ya mashamba. Inavyofahamika Kenya nzima, kama kuna mahali kulikoathirika zaidi na masuala ya mashamba ni sehemu ya Pwani. Mashamba yao yamenyakuliwa kwa dhuluma kupitia vyeti vya ardhi bandia. Toka jadi, watu wameandika vyeti vya ardhi gushi na kuja kufurusha wakaazi wa Pwani bila kujali maslahi yao, makaburi, makanisa au misikiti iliyopo maeneo yale.

Kwa upande wa Taita Taveta, najumuika na---

(Sen. (Dr.) Oburu walked into the Chamber)

Kiongozi wa chama changu cha kisiasa anapita. Kwa hiyo, ni lazima nimpatie heshima yake.

Bw. Naibu Spika, pia watu wa Taita Taveta wameathirika. Kwanza, kuna wanyama wanaoingia kwa mashamba kama tunavyoona. Vilevile, mashamba yao yamechukuliwa na watu wanaojua wazi vitendo wanavyofanya ndani ya Wizara ya Ardhi ni ukorofi, wizi na ufisadi. Utakuta kwamba yote yaliyofanyika kwa wakaazi wa Marungu, Taita Taveta, ni dhuluma.

Katika maono tuliyo nayo, ni vyema Wataita wenyewe wanaoishi katika yale maeneo waweze kupewa hayo mashamba. Jukumu hilo hivi sasa likiwa katika Seneti, tuna imani ya kwamba kupitia kwa Mwenyeketi wa Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili, ndugu yetu, Mohammed Faki, atie mkazo zaidi kuona ya kwamba baada ya hapa, haya mambo sio ya kulala, ni ya kuendelea mbele ili kuhakikisha kwamba watu wa Taita Taveta wamepata haki yao.

Vilevile, mbuga nyingi sana, kwa mfano, kule Kilifi, hususan upande wa Mtwapa, Shariani, Vipingo, Kilifi Gold na hatimaye uende juu kabisa mpaka Kilifi North, Msabaha huko kwote na Malindi hadi mbele ya Marafa ambayo ni eneo la Magarini, mashamba haya yamechukuliwa kwa hali ya dhuluma. Hii ni kwa sababu wale wanaoishi pale, wanaweza kuwa hawana ile azma ama akili ya kuweza kufikiria ya kwamba, hapa tunapoishi, tulipozaliwa na ambapo makaburi ya babu zetu ziko, hapa ambapo tukiangalia hivi, hatuna kwingine kwa kwenda katika Kenya hii, isipokuwa papa hapa ambapo kuna makanisa yetu, mashule yetu na makao yetu tunapoishi kama mji; itakuwa ni jambo la kusikitisha hivi leo kuona kwamba watu hao wanafurushwa bila huruma.

Wale ambao tunaweza kuwalaumu zaidi ni kuwa kuna mapolisi maalum ambao wamejihusisha sana na mambo ya mashamba. Ikifika wakati wa kuwafurusha wakaaji au wenyeji katika ardhi zao, utawaona polisi hao; watatoka hata kama ni Mtwapa waende hadi Malindi, Magarini na kwingineko lakini ndani ya Kilifi County utapata hao ndio wamekuwa majabali sasa wa kufukuza wale *locals* kwa sababu wao wanasema, wametumwa, na wana stakabadhi za kortini. Wakati mwingine hata wale askari hawaangalii kama zile *orders* wamepewa kama ni bandia. Mara nyingi inatokea kwamba mawakili wameenda kortini wakiwatetea wale wanavijiji, wanaopata orders ya kwamba, hii tite haonekani ndani ya Wizara ya Ardhi.

Kwa hivyo, tunataka kuweka mkazo; dalili hizi ambazo Kamati hii ya Seneti ya Ardhi ikiongozwa na ndugu yetu Mohammed Faki Mwinyihaji, ni kwamba kuwe na mikakati mizuri ili watu waitwe na waulizwe maswali. Wakiweza kujibu sawa, ikionekana kwamba kulikuwa na dhuluma na mashamba yao yakapewa watu wengine ama watu wakatoa zile stakabadhi bandia, basi suala kama hili litatuliwe na Wizara ya Ardhi kuona ya kwamba watu wanaoishi pale wamerejeshewa ardhi zao.

Asante, Bw. Naibu Spika.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Thank you. I now call upon the Mover to reply.

Sen. Faki: Thank you, Mr. Deputy Speaker, Sir. I thank Sen. Chimera for his able contribution to this Motion. I also thank our Minority Leader for his contribution to this Motion. I thank Sen. Mwaruma for seconding the Motion. Sen. Mwaruma is not only a Member of the Committee, but also the area Senator. When we visited Taita Taveta because of this particular petition, he was very helpful in explaining the issues to us, as a Committee.

Mr. Deputy Speaker Sir, as you are aware, the land issue in the Coast is very funny. We have seen instances where people are being evicted just because somebody in Nairobi allocated the land to the wrong person. The other day we were in Meru and we saw for ourselves the issues that were there, the land which was reserved for the public utilities was being appropriated by the church. However, I am glad the church was willing to come, sit down and discuss the issue with us.

In Jomvu, Jomvu Kuu area, the Methodist Church, took about 170 acres of land. Right now, they are subdividing and selling it to third parties yet initially the land was meant for use by the church. How does a church become a land broker?

This is all a matter of addressing the land historical injustices. The NLC should do more than just saying that we are handicapped. Although they have many cases right now, they have about 1,500 cases, and I understand their time is coming to an end next month, but that does not stop them from working hard to make sure that some of these cases are resolved as soon as possible.

I thank you, Mr. Deputy Speaker, Sir. I beg to move that under Standing Order No.66(3), putting of the question be deferred to the next date.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Your request is granted, Chairperson of the committee.

(Putting of the Question on the Motion deferred)

Next Order.

MOTION

ADOPTION OF REPORT ON PETITION ON DELAYED ALLOCATION OF LAND TO MWANDABUSI LAND SQUATTERS, KISII COUNTY

Sen. Faki: Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to move-

THAT, the Senate adopts the Report of the Standing Committee on Land, Environment and Natural on a Petition to the Senate by representatives of Mwabundusi land squatters in Bobaracho Ward, in Kisii County concerning delayed allocation of alternative land by way of re-settlement or compensation for the ancestral land that was alienated by the Government of Kenya for creation of the Kisii Agricultural Institute and Kisii Farmers Training Centre, laid on the Table of the Senate on Tuesday, 7th October, 2025

Mr. Deputy Speaker Sir, this is another case of land historical injustice that was presented to this Senate by the Mwabundusi land squatters residing in Bobaracho Ward of Kisii County. The land was alienated by the government for the purposes of the Kisii Agricultural and Livestock Organisation (KALRO), formerly KARI, and the Kisii Farmers Training Centre (KFTC). Initially, the squatters lived on the land in the early 1960s.

The petitioners the Senate to direct the NLC to conduct independent and accurate audit to examine the actual acreage occupied by KALRO and KFTC and number two, ensure expeditious allocation and resettlement of the petitioners on available public land as compensation for the alienated ancestral land.

The KALRO land in Kisii has been in the eye for many years. In fact, several high-profile politicians coming from that region have been beneficiaries of allocations. This include, a portion that was allocated to Jared Benson Kangwana, who in fact obtained judgement in his favour for that particular portion. There were other matters which are still pending in court and, therefore, we could not delve deeper into this land.

Mr. Deputy Speaker Sir, although they had petitioned the NLC which did not hear their cases because of the termination and maybe retirement of the commissioners.

The Committee visited the land and they had an engagement with the squatters. Part of the land is occupied by KALRO and KFTC. The other part is still vacant. However, KALRO and Kisii Farmers Training Centre (KFTC) still need land to undertake their activities.

The Committee recommended that the NLC goes back to the ground, with the assistance of local leaders, community and members of Mwabundusi Squatter Society, to do a survey to ascertain the actual land that is occupied by KALRO and KFTC.

We also recommended that if there will be any available land, apart from the land that is reserved for KALRO and KFTC, the land should be considered for allocation to the squatters who originally occupied that land. However, that is subject to whether the land that is available is enough for KALRO because we know that in the coming days, research will be required in order to uplift the agriculture potential of Kisii County. It will also be required to bring in new and innovative farming ideas to the farmers. Therefore, training will be necessary for farmers, so that whatever is being researched can be passed on to the farmers in order for them to improve their yields due to new and modern farming techniques.

Mr. Deputy Speaker, Sir, having moved this Motion, I request Sen. Beatrice Ogola to second.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Proceed, Sen. Beatrice Akinyi.

Sen. Ogola: Mr. Deputy Speaker, Sir, I am honoured to second this Motion as moved by my Chairman, Sen. Faki. As I second, it is important to note the non-responsive nature of the NLC in all these petitions.

Sometimes back on this Floor, the Committee on Land, Environment and Natural Resources was reminded that we had 13 petitions pending before the Committee. I want to say from the start that Kenyans had a lot of hope in the work of the NLC. However, for most petitions that we deal with, we are unable to move with speed as expected by petitioners because the NLC has been slow. It could be that they do not have the capacity to deal with the expectations of Kenyans efficiently and effectively. If that is not the case, they need to come and tell Kenyans or Parliament clearly that they do not have resources to accomplish the mandates that Kenyans bestowed on them.

This is a petition that we dealt with and the committee went to the ground. As the Chair stated, land issues must be attended to. It is the responsibility of the NLC to manage public land on behalf of counties and the national Government. Therefore, we have a lot to expect from them.

Historically, we know that a number of places have a lot of injustices that have been meted on them. Those are the core mandates that Kenyans bestowed on the NLC.

Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to second.

(Question proposed)

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): I will allow a few Senators time to make comments, starting with Sen. Richard Onyonka.

Sen. Onyonka: Bw. Naibu Spika, kwanza, ningependa kutoa shukrani zangu kwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili. Ombi la wakaazi wa

Mwabundusi ambao shamba lao lilichukuliwa na Serikali karibu miaka 80 iliyopita ni jambo ambalo limekuwa likiwakera.

Tulipokutana na wananchi hao hapa Nairobi kwa mara ya kwanza kwa sababu baadhi yao ni viongozi kule mashinani ambao tunajuana nao na wengi wao wamestaafu, walisema kuwa swala la shamba hilo limekuwa likiwakera na hawajui la kufanya. Walileta *petition* hapa katika Seneti kwa sababu mbeleni NLC ilikuwa inachukua muda mrefu.

Ningependa tuangazie jambo hili katika Seneti na ningependa Sen. Faki alifuatilie. NLC ikijua kuwa kuna jambo ambalo wananchi wanataka liangaziwe kuhusu shamba, hawachukui muda mfupi kusuluhisha shida hiyo.

Hapa nchini kuna Katiba inayotumika. Ningependa kutoa shukrani zangu kwa Mzee Raila kwa kusema kuwa kulihitaji taasisi ambayo itasaidia kusuluhisha mambo ya mashamba kihistoria nchini Kenya.

Jambo la pili ni kwamba kwenye shamba hilo ambalo liko katika Mji wa Kisii, kuna Idara ya Serikali ijulikanayo kama Kenya Institute of Highways and Building Technology (KIHBT) inayohusika na mambo ya ujenzi. Vilevile kuna chuo cha National Youth Service (NYS) na Veterinary Department. Vilevile, Kisii Bottlers Limited ilikuwa hapo. Sasa hivi kuna cancer centre hapo.

Kabla ya *petition* hii kuletwa, tulikuwa tunajaribu kuangalia shida iko wapi. Baadaye wazee hao walipokuja, walisema kuwa hawataki kuhusika katika kuondoa KALRO, KIHBT na Veterinary Department. Hata hivyo, walisisitiza kuwa babu zetu walikuwa na shamba ambalo lilikuwa ekari 480. Shamba ambalo walifaa kupeana kwa Serikali lilikuwa ekari 86. Makubaliano hayo na kila kitu kipo.

Baada ya wazee hao kwenda kwa NLC, tulikaa kama Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili. Ningependa kusema kuwa nafurahia kwa sababu kamati ya Seneti hii inayohusika na mambo ya mashamba imesema kuwa lazima Idara inayohusika na survey iende kule Kisii kufanya survey ili tujue shamba lile ambalo lina maskwota na Idara za Serikali lilikuwa ekari ngapi.

Jambo la pili ni kuwa Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili imesema kuwa uchunguzi ufanywe kuhusu Idara ya Mifugo ambayo iko katika shamba hilo ili tujue shamba lao ni ekari ngapi.

Mwisho, Kamati ilipendekeza kwamba shamba ambalo litabaki bila wakaazi, kwa sababu ukienda pahali panaitwa Itezezi ama Mwabundusi, utapata kuna karibu ekari 50 ambazo ni uwanja tu, hakuna mtu anaishi hapo ilihali idara zote za serikali ziko kwa zile ekari 85. Hata the Kisii National Institute iko kwenye hiyo shamba.

Hawa wazee walisema kwamba hawataki kujihusisha na hayo mashamba ambayo yako na idara za kiserekali kwa sababu wanajua uzuri wa idara za Serikali. Waliuliza kwa afueni yao kwamba survey ifanywe na hii Kamati imekubali kwamba survey itafanywa. Kamati pia imewashauri viongozi wote wanaohushishwa kuketi chini baada ya hawa waze wamekaa chini na National Land Commission (NLC) ili survey ifanywe.

Bw. Naibu Spika, sijui kama Mhe. Faki alijua hilo, lakini, Kamati iliporudi hapa Bunge, walienda wakafanya survey na maafisa wa Serikali. Nadhani hiyo ripoti imeisha.

Ingawa idara inayoshughulika na mambo ya ardhi, the NLC imejaribu sana, kujihusisha, Kenya yetu bado ina mambo mengi kuhusu mashamba. Kuna mashamba

ambayo yamenyakuliwa, mengine yako na title deeds zaidi ya moja, mengine ni mashamba ya shule ambayo yamenyakuliwa na mabwenyenye na wakajenga mahoteli na vitu kama hivyo.

Ombi langu ni kuwa, NLC ijue kwamba iliundwa lengo lake likiwa kusuluhisha shida na vita ambavyo viko pale mashinani. Wakijihusisha vilivyo, hakutakuwa na maskwota na pia unyakuaji wa mashamba. Wananchi hata hawangependa kupeleka hizi kesi kotini kwa sababu kesi za mashamba huchukua zaidi ya miaka kumi kusuluhishwa.

Mhe. Faki, umefanya kazi nzuri katika Kamati yako ya Ardhi, Mazingira na Maliasili.

Bw. Naibu Spika, nilisikia ndugu zangu wakisema kuwa kuna mambo fulani wangependa serikali ijihusishe nayo. Serikali inafaa kuhakikisha kwamba kila mtu, awe Seneta, gavana hata Rais amejisajili na Ardhisasa ili tuweze kujua ni nani ana shamba halali na nani hana. Tukifanya hivi, tutakuwa na rekodi na kupata suluhu wakati kuna vita ama watu hawaelewani. Vile mnavyosema kwamba hii serikali inajali mambo ya watu maskini, lazima ijihusishe vilivyo kwa kuhakikisha kwamba hili jambo la mashamba litapata suluhu na mambo ya Mkenya kuitwa skwota kwao yaishe.

Nikimalizia, ningependa kumshukuru ndugu yangu, Mwenyekiti, Sen. Faki, umefanya kazi nzuri. Natoa heshima zangu sana kwa hii Kamati ya Bunge kwa kuwapea afueni hawa wazee ambao wamesha kustaaifu. Watatu wa wale waliokuwa hapa wana zaidi ya miaka 80. Ni heshima sana, na najua hata wajukuu wao watafurahia kwa sababu at least, justice imekuwa served.

Nashukuru sana, Bw. Naibu Spika.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Asante sana.

Naomba mwasilishi wa Hoja aweze kujibu.

Sen. Faki: Asante, Bw. Naibu Spika. Naona unajitahidi kwa Kiswahili kwa sababu juzi tulipokuwa Meru, ulipata shida kutamka “utepetevu”. Asante kwa kunipa fursa hii.

Namshukuru Sen. Beatrice Ogola kwa kuunga mkono Hoja hii. Vilevile namshukuru Sen. Onyonka ambaye alihudhuria mikutano na vikao ambavyo tulifanya na watu wake wa Kisii kuhusiana na swala hili.

Ni kweli kwamba NLC haifanyi kazi yake kwa haraka inavyostahili. Kwanza, wanashida ya bajeti na shida zingine za kimsingi zinazowazuia kufanya kazi zao kikamilifu. Kwa mfano, ripoti zetu nyingi zilichelewa kwa sababu NLC haikuja kwenye Kamati kutueleza mambo kuhusiana na maswala tofauti tofauti. Lakini katika kikao cha mwisho na mwaneyekiti, alithibitisha kwamba atayatilia nguvu maswala hayo ili ripoti zetu zisichelewe na mahitaji ya wananchi ya uchunguzi yasicheleweshe.

Bw. Naibu Spika, ripoti hii ikitekelezwa, itahakikisha kwamba yale matatizo ambayo hawa wananchi mabundusi wameweza kuona kwamba haki imetendeka. Ardhi ambayo ilikuwa imetengewa maskwota wote ilikuwa ekari 400 na Kenya Agricultural and Livestock Research Organisation (KALRO) walisema kwamba yao ni ekari 100. Kwa hivyo, kuna karibu ekari 300 ambazo zikigawanywa, wale ambao wameishi pale kwa muda wa mababu na mababu, watapata afueni.

Vilevile kama Kamati, tutaweza kusimamia Wizara pamoja na NLC ili kuhakikisha kwamba hizi ripoti zote ambazo zimeletwa mbele ya Bunge, zimetekelezwa na kwa muda unaofaa.

Asante, Bw. Naibu Spika.

Naomba uamuzi wa Hoja uairishwe hadi siku za usoni kulingana na Kifungu 66(3) cha Kanuni za Senate.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Mwenyekiti, ombi lako limekubalika.

(Putting of the Question on the Motion deferred)

Let us move to the next Order.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Mazingira na Maliasili.

MOTION

ADOPTION OF REPORT ON PETITION ON RECOGNITION OF LAND OWNERSHIP RIGHTS AND REDRESS OF HISTORICAL LAND INJUSTICES IN MOMBASA COUNTY

Sen. Faki: Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to move-

THAT, the Senate adopts the Report of the Standing Committee on Land, Environment and Natural Resources on a Petition to the Senate by Mr. Nagib Shamsan and others concerning recognition of land ownership rights and redress of historical injustices in Mombasa County, laid on the Table of the Senate on Tuesday, 7th October, 2025.

Mr. Deputy Speaker, Sir, Mombasa and the Coast region has had a unique land ownership tenure which is also known as houses without land; where I own the house, but the land belongs to somebody else. This kind of ownership came up as a result of the historical nature of the coastal strip where land was in the trusteeship of the Sultan of Zanzibar. When the Sultan relinquished the coastal strip to the Government of Kenya, there were no efforts put in place to rectify this problem.

Apart from the few pieces of land that were allocated to people, most of the land remained in the hands of the Government. At the same time, Government functionaries took advantage of that and allocated themselves a lot of land in the Coast region at the expense of the citizens of that region. Therefore, you will find that in most areas such as Kisauni, Chagamwe and even the island, many people do not have title deeds for the houses that they own.

In the 1980s, the late President Moi declared an embargo that all the people who are owning land within the island, will only sell the land to the people who own houses. At that time, the land was going for about Kshs30,000 for those on the main road and Kshs15,000 for those behind the main roads. Many people took advantage of this and were able to regularize their position. However, in places like Kisauni and Chagamwe, this tenure system still persists.

Mr. Deputy Speaker, Sir, currently the land owners are imposing exorbitant land rent on the people owning these houses. They will wake up in the morning and say that they increasing the monthly rent from Kshs500 to Kshs1,500. Some are even asked to pay Kshs10,000 or Kshs15,000. Last week, I saw some notices which were served on some residents of the island where they are being asked to either pay Kshs6.5 million for their plot or pay rent at a sum of Kshs6,000 per month, for that portion which sometimes measures about 50 by 40 or 80 by 100.

Mr. Deputy Speaker, Sir, this is a continuing problem. People have not been able to develop their houses because whenever they want to, they still have to go back to the land owner for consent which is awarded on the basis of the value that one wants to put on that land. For instance, if you are building a house of Kshs1 million, you are supposed to part with Kshs100,000 as a consent fee to the land owner and on top of that you continue paying the land rent. The only document they normally have is the building plan, which is signed by the land owner and the developer, so that if you want to go to the bank, you cannot access to credit or if you want to bond or bail somebody who has been charged with a criminal offence, you cannot take that document to court for issuance of the bail. In a nutshell, you cannot use that document at any other place apart from your relationship with the land owner.

Mr. Deputy Speaker, Sir, we investigated this. We visited Mombasa and had presentations from the National Land Commission (NLC) and Mr. Najib Shamsan and Mr. Abdullahi Farah, who is an elder resident in Mombasa. We had a serious consideration. In fact, we discussed these issues with the NLC and we were able to see what could be done in order to resolve these issues. The NLC also did their own investigation and they presented their report to the Petitioners on the historical land injustices in the last month of September in Mombasa.

Mr. Deputy Speaker, Sir, we are recommending the following-

(1) That the NCL should expedite all the investigations into historical land injustices claims in Mombasa and make a final determination within three months upon adoption of this report by the Senate. I am aware that they have already made their recommendations and their recommendations are twofold-

Number one, that the national Government comes into acquire the land which is owned by these private land owners and redistribute it to the people who are residents on those portions of land.

In the meantime, pending the Government acquiring this land for purposes of resettling those people, there should be no evictions in Mombasa and the coast region in general.

Two, that, the Mombasa County Government to investigate matters of alleged illegal subdivisions of land and streamline the remittance of land rates by the absentee landlords.

Most of these landlords do not pay land rates that are due to the County Government of Mombasa. The County Government has also allowed subdivisions even when they are people with questionable documents. For instance, the land at Mwembe Kuku was one land parcel, but it was subdivided into portions, all of which have now been valued by the landowners at Kshs5 million per plot. These amounts, are very

exorbitant to the people who own those houses because they are not be able to buy those houses and the landowner is at liberty to sell to any other willing buyer.

Three, the Ministry of Lands and Public Works and the NLC should come up with a reasonable land valuation criterion to enable the landowner to charge the lessee and the tenants fairly.

Mr. Deputy Speaker, Sir, the landowner does not use any formula of charging the land rent. They wake up one day and say, we are issuing a notice that effectively from 1st November we are going to charge you Kshs3,000 per month for your plot. So, this one has to come to a stop, because already these people have been paying the rent for the many years and maybe they have not been offered any service by the landowner.

Four, the NLC undertakes a thorough analysis to document the challenges and propose context-specific interventions that will inform future policy reforms and legislative amendments to ensure equitable land distribution and conflict resolution.

These proposals are to be shared with the Committee on or before the 31st December.

Mr. Deputy Speaker, Sir, here we are addressing the issue of policy because at the moment the Government does not have any policy on what happens to these people who have been owning houses, but they do not own the land. Can the Government come up with a policy that they acquire the land from the landowner and then allocate it to the house owners at a reasonable price, so that people are settled and they obtain titles for the land that they own?

Mr. Deputy Speaker, Sir, this is the report on the land historical injustices. The Committee has taken the time to visit Mombasa to see for themselves the problems that these issues have generated. Previous attempts were done. I remember in the years between 2003 and 2007, there was a Committee which was established by the Ministry of Lands, Public Works, Housing and Urban Development headed by Prof. Kivutha Kibwana, who was then the Minister for Lands, Public Works, Housing and Urban Development, to deal with the issues of these historical land injustices in the coast.

Mr. Deputy Speaker, Sir, I beg to move and ask Sen. Mwaruma to second this Report.

I thank you.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Sen. Mwaruma, please proceed.

Sen. Mwaruma: Thank you, Mr. Deputy Speaker, Sir, for this opportunity to second this Motion on the report on historical land injustices in Mombasa. Being a resident of Mombasa, I am well privy and apprised of this issue of historical land injustices in Mombasa and the issue of people who have built houses, but do not own the land. This is an issue of historical land injustices and it should be addressed by the NLC. I want to also decry the complacency and the lack of assertion by the NLC to resolve the issues of historical land injustices which are rampant within the coast region.

Mr. Deputy Speaker, Sir, I wanted to comment about the Mwabundusi land, but you did not give me the opportunity. It is an issue where a historical land injustice claim has been laid within the NLC, but the NLC is not keen on addressing that injustice. Back to Mombasa, there are many people who are suffering and the NLC can apply themselves judiciously to resolve this issue.

Mr. Deputy Speaker, Sir, these issues are not only unique to Mombasa. Even in Taita Taveta, there are areas where Government institutions have taken land belonging to the public. We have cases in Taita Taveta where the National Transport and Safety Authority (NTSA) has taken land. They are claiming that land is theirs, yet the people have built houses and now they want to evict those people.

We have a case where the prison department has taken a big chunk of land at a place called Ore in Voi, where the people of Ore are farming, but because there was a Gazette Notice in the 1970s where the Government gave land to the prison department, the prison department is claiming that land and they have started constructing houses without a title deed. The money that they are using was given by the NLC as compensation because of construction of the Standard Gauge Railway (SGR).

The question we have been asking ourselves is that: Is it proper for the Government to compensate a Government entity land? Therefore, the issues of land in Mombasa and the Coastal region are valid and the Chairperson has explained well that they need to be addressed by the NLC and the Ministry of Lands, Public Works, Housing and Urban Development.

Mr. Deputy Speaker, Sir, I am happy to note that the Government has gone ahead and provided a framework of purchasing some of the land and settling the residents. This is an issue we will laud, but we need expedition of that process, so that the people of Mombasa can live comfortably. We have a house that was built by my family in 1970 in Mombasa, but up to date, we are still paying land rates for all those over 35 years. I hope the recommendations of this report will be expedited and implemented, so that historical land injustices of Mombasa are addressed.

I thank you.

(Question proposed)

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Sen. Beatrice Akinyi Ogola.

Sen. Ogola: Mr. Deputy Speaker, Sir, I rise to support the Motion as moved by Sen. Faki, who is the Chairperson of the Committee on Lands, Environment and Natural Resources and seconded by the Senator for Taita Taveta, Sen. Mwaruma.

My contribution will put an emphasis on the role Kenyans expected from the NLC. This Commission in its structure to address historical injustices and the mandate that was given to it in the Constitution and the Land Act needed to have vibrant offices in the counties. The NLC should have devolved offices in the counties that are fully constituted and not run by one-man officers in the name of county coordinators that they have in the counties.

This is because the issues that the NLC are dealing with are many and not limited to historical injustices. Initially when this Commission was constituted, they had County Land Boards as a decentralized structure of the NLC that had the coordinator and other professionals like surveyors or adjudication officers. That made it possible for the NLC to deal with the many issues. However, we have a situation where the NLC runs from the national level and only keeps one officer to just send reports. That is not the dream Kenyans had.

Disclaimer: *The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Director, Hansard and Audio Services, Senate.*

Mr. Deputy Speaker, Sir, I support this Motion and say that the historical injustices that have been presented here must be attended to in time. We have proposals that have been brought out in the Report. One of them is a proposal by the NLC that the Government should acquire land in order to resettle some of the petitioners.

If we have to go this way, I suggest that in the acquisition process, evaluation must be done properly and before land is picked by the Government to settle, compensation must be done well in advance. We have projects everywhere in this country where projects are undertaken, land has already been acquired by the Government, but after that, our people cry for compensation for a long time. The other option that was proposed here is that the legal subdivisions must be looked into and a thorough investigation done by the NLC.

The issue of investigation is crucial because if they were to do investigations, the findings would help the NLC solve other related historical injustices. I also would like to emphasize that we must look at the capacity of the NLC in terms of resources and the professionals they have, so that they can address the issues raised by Kenyans, the Senate and elsewhere because that is the main reason that the NLC was constituted.

I thank you, Mr. Deputy Speaker, Sir.

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri): Having no other Member interested in contributing, I call upon the Mover to reply.

Sen. Faki: Asante, Bw. Naibu wa Spika, kwa kunipa fursa hii. Dhuluma za historia kwa masuala ya ardhi katika eneo la Pwani na Mombasa ni jambo limekuwa donda sugu kwa wakaazi wa huko. Vilio vya watu wa Mombasa ni kwamba, suala hili la umiliki wa nyumba bila ardhi, ni jambo ambalo ni lazima Serikali iingilie kutatua kwa sababu ina uwezo na rasilimali za kutosha kuhakikisha wale ambao wanamiliki ardhi, watalipwa fidia au ridhaa ili watoe ardhi hizi kwa wananchi wa kawaida.

Tunajua Serikali imetoa mikakati na maelezo kwamba watanunua ardhi hizi. Lakini, kwa miaka miwili mfululizo, zile pesa zinazotengwa kwa maswala haya ya ardhi zinatumika kwa miradi ingine inayotokea ya serikali. Ni kama serikali haina nia ya kuimaliza tatizo hili la ardhi kikamilifu katika maeneo ya Pwani. Kuna wengi wako pale na serikali ina uwezo wa kulipa lakini kwa sababu hakuna mfumo ambao utaleta usawa au haki kwa pande zote ili mwenye ardhi asipoteze ardhi yake bila malipo na yule mwenye nyumba asidhulumiwe kwa sababu amewekeza katika nyumba ile kwa muda mrefu.

Hii NLC ingeleta pamoja wenye ardhi na wenye nyumba, kwa mfano, kule Kisauni, wawe na kauli moja kuhusiana na dhamani ya zile ardhi ziko katika eneo lile. Changamwe pia pawe na mfumo kama huo ili watu waelewane na waweze kulipa kiwango ambacho kinaridhisha kwa kila upande.

[The Deputy Speaker (Sen. Kathuri) left the Chair]

[The Temporary Speaker (Sen. Veronica Maina) in the Chair]

Bi. Spika wa Muda, naomba Bunge hili likubali ripoti hii na uamuzi wa uhairishwe kuambatana na Kifungu 66(3) cha Kanuni za Seneti hii mpaka siku nyingine.

(Putting of the Question on the Motion deferred)

The Deputy Speaker (Sen. Kathuri: That request is granted.

Hon. Senators, there was clear guidance earlier on that after dispensing with the Motions up to Order No.21, we go back to Order No.17.

BILL

Second Reading

THE COUNTY OVERSIGHT AND ACCOUNTABILITY BILL (SENATE BILL NO. 3 OF 2024)

(Sen. Olekina and Sen. Kisang on 08.10.2025)

(Resumption of debate interrupted on 28.10.2025 - Afternoon Sitting)

The Temporary Speaker (Sen. Veronica Maina): Hon. Senators, we are now at resumption of debate on The County Oversight and Accountability Bill (Senate Bill No.3 of 2024). Sen. Beatrice Ogola, you had a balance of nine minutes. I do not know whether you still want to pursue your minutes or cede ground to another Senator to proceed. You may take the Floor.

Sen. Ogola: Thank you, Madam Temporary Speaker. I will only use the next two minutes and cede the rest to my colleagues.

I support this Bill primarily because it will improve efficiency, as I indicated and the fact that it emphasizes on the access to information by members of the public.

It will enhance public participation because it even mentions the improvement of public participation facilities. However, I indicated yesterday that the lack of adequate and quality public participation is not necessarily due to lack of facilities, but because of the non-structured way in which it has been undertaken. For us to get quality public participation, we must also include the education of members of the public, so that they also participate in oversight of the projects.

I support.

Sen. Mwaruma: Thank you, Madam Temporary Speaker, for this opportunity to support this very important Bill, The County Oversight and Accountability Bill, co-sponsored by Sen. Kisang and Sen. Ledama Olekina, the Senator for Narok.

In the previous Parliament, we had opportunity to go through this same Bill, but it died on the way. I am happy that he was able to bring it back.

In the new Constitution of Kenya, 2010, devolution is the best thing that we ever gave to ourselves. I laud the late former Prime Minister, Rt. Hon. Raila Amolo Odinga, who was the main proponent of the Constitution and his support for devolution even after the Constitution was promulgated. We will forever, as small communities, remember him

for his support for devolution, which then devolved money and power from the centre to the counties.

This Bill is informed by the fact that when we appropriate money to the counties, we do not have adequate mechanisms of doing oversight. There are gaps in all the structure of oversight and its whole ecosystem in the counties, for the county governments, which is what has informed Sen. Olekina to bring this Bill. Primary oversight is supposed to be undertaken by the county assembly, but the way the assembly is formed, it is not able to do proper oversight.

